**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**OFISI YA RAIS**

**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**

# MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA TANO KATIKA SHULE ZA SEKONDARI ZA SERIKALI TANZANIA

**Juni, 2025**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**OFISI YA RAIS – TAMISEMI**

Namba za Simu
Mkuu wa Shule: 0783 273 538
Makamu Mkuu wa Shule: 0784 169 094
Matron/Patron: 0684 982 878

**Shule ya Sekondari Nakaguru**
**S. L. P 611**
**Ifakara**
**Tarehe: April 30, 2025**

**Mzazi/Mlezi wa Mwanafunzi**
**………………………………………….……..**
**S. L. P ……………………………………..**
**……………………………………..……….**

Yah**: MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA TANO KATIKA SHULE YA SEKONDARI NAKAGURU HALMASHAURI YA WILAYA YA MLIMBA MKOA MOROGORO MWAKA 2025**

**1.** Nafurahi kukutaarifu kuwa mwanao amechaguliwa kujiunga na Kidato cha Tano katika Shule hii mwaka 2025/2026 na atasoma tahasusi ya CBG/ PCB/PCM

**MAHALI SHULE ILIPO**

Shule ya Sekondari Nakaguru ipo katika kata ya Mchombe tarafa ya Mngeta Halmashauri ya wilaya ya Mlimba karibu na eneo pekee duniani lenye vyura wanaozaa na sehemu wanayofua umeme kwa jina la Kihanzi Hydroelectric plant.

a) Nauli ya basi kutoka Morogoro mjini hadi Mlimba Tsh. 25,000, kumbuka kushuka Shule ya Sekondari Nakaguru iko barabarani.
b) Kutoka Dar-es-Salaam, panda train shuka station ya Mngeta, kisha chukua bodaboda kwa 1,000 au 2,000 usiku kufika shuleni.

Muhula wa Masomo kwa kidato cha V unaanza tarehe **08/07/2025**, hivyo mwanafunzi anatakiwa kuripoti shuleni tarehe **07/07/2025** na masomo yataanza tarehe **08/07/2025** mwanao anatakiwa kuwahi kufika asichelewe masomo.

**2. Mambo muhimu ya kuzingatia:**

**2.1 Sare za Shule**

i. Sare ya shule hii ni Suruali mbili rangi ya dark blue (blue black), zenye marinda mawili (upana chini nchi 16 pia iwe na "turn up"

ii. Mashati mawili meupe mikono mifupi aina ya tomato.

iii. Sare ya Michezo ni bukta 1 na jezi 1 rangi kijani au track suit ya kijani.

iv. Viatu vya shule ni vyeusi vya kufunga na kamba vyenye visigino vifupi;

v. Soksi jozi mbili nyeusi

vi. Mkanda mweusi wa ngozi wa kuvalia suruali;

vii. Sweta moja rangi ya dark blue.

viii. Nguo za kushindia ni suruali ya khaki na tshirt itapatikana shuleni kwa Tsh. 15,000/=

**2.2 Mahitaji mengine muhimu ambayo mwanafunzi anapaswa kuja nayo shuleni:**

i. Madaftari 10 aina ya counter books quire 2 au 3 au zaidi.

ii. **Ream paper (A4)** mbili (2) kwa mwaka;

iii. Vitabu vya masomo ya tahasusi husika (*orodha imeambatanishwa*)

iv. Dissecting kit kwa wanafunzi wanaosoma Biology;

v. Scientific Calculator;

vi. Njoo na godoro la kulalia lenye upana futi mbili na nusu (2.5), urefu futi sita (6) unene kuanzia inch 3 na kuendelea.

vii. Njoo na shuka mbili rangi ya light blue, mosquito net 1, foronya ya kulalia.

viii. Nguo za ndani za kutosha;

ix. Vyombo vya chakula (sahani, bakuli, kijiko na kikombe);

x. Ndoo 1 ndogo (lita kumi) ya kuogea na kufulia pamoja na dumu la litre 5 la kutunzia maji ya kunywa.

xi. Kwanja 1 na ufagio wa nje kwa wanafunzi wa tahasusi ya PCM

xii. Jembe 1 lenye mpini kwa wanafunzi wa tahasusi ya CBG.

xiii. Reki 1 na ufagio wa ndani kwa wanafunzi wa tahasusi ya PCB

xiv. Sabuni ya chooni lita 2 kwa mwaka kwa wanafunzi wa tahasusi zote.

xv. Picha nne (4) za wazazi na ndugu wa karibu wa mwanafunzi wanaoweza kumtembelea mwanafunzi shuleni pamoja na namba zao za simu.

**2.3 Michango mbalimbali**

| Na | Aina ya Mchango | Kiasi |
|---|---|---|
| 1. | Mchango wa Uendeshaji wa Shule | 65,000/= |
| 3. | Tahadhari | 5,000/= |
| 4. | Nembo | 5,000/= |
| 5. | Kitambulisho cha Shule | 5,000/= |
| | **Jumla** | **80,000/=** |

Malipo yote yafanyike kwenye akaunti ya **Shule ya Sekondari Nakaguru NMB Na: 21601200068**

## 3. Sheria na Kanuni muhimu za Shule

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa Sheria ya Elimu Na. 25 ya mwaka 1978 na kama ilivyo rekebishwa kwa Sheria Na. 10 ya mwaka 1995. Aidha, inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia yenye dhamana ya elimu na Ofisi ya Rais – TAMISEMI yenye jukumu la usimamizi na uendeshaji wa elimu nchini. Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yanafafanuliwa kwa maandishi na utapewa nakala yake mara baada ya kuripoti shuleni. Mambo hayo ni pamoja na;

### 3.1 Sheria na Kanuni za Shule

i. Heshima kwa viongozi, wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima;
ii. Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ya shule;
iii. Kushiriki kwa kikamilifu masomo ya usiku (preparations);
iv. Kuwahi katika kila shughuli za shule utakazopewa;
v. Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo ya kuwepo ndani na nje ya mipaka ya shule.
vi. Kutunza usafi wa mwili, mavazi na mazingira ya shule;
vii. Kuvaa sare husika ya shule wakati wote.
viii. Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote;
ix. Kutunza mali za shule;
x. Ni marufuku mwanafunzi kumiliki vifaa vyenye ncha kali na dawa bila idhini ya daktari au mwalimu wa malezi.
xi. Mwanafunzi haruhusiwi kubadili dini wala kumshawishi mwanafunzi mwenzake kubadili dini wawapo shuleni.

**MUHIMU:**

- **Mwanafunzi hapaswi kuja na simu shuleni kwa namna yoyote ile, na hakuna mtumishi anayeruhusiwa kutunza simu ya mwanafunzi;**


- **Mwanafunzi awapo shuleni atatakiwa kulala kwenye bweni alilopangiwa na kitanda alichopangiwa. Ni marufuku mwanafunzi kulala kitanda kimoja na mwenzake au kuishi kwenye bweni ambalo hakupangiwa. Kitanda kimoja kitatumika na mwanafunzi mmoja tu;**

- **Mwanafunzi ataruhusiwa kurudi nyumbani kwa ruhusa na kibali maalum toka kwa Mkuu wa Shule. (Msiba au Ugonjwa**).

**3.2 Makosa yatakayosababisha Mwanafunzi kufukuzwa Shule ni pamoja na:**

i. Wizi;
ii. Kutohudhuria masomo kwa zaidi ya siku 90 bila taarifa/utoro;
iii. Kugoma na kuhamasisha mgomo;
iv. Kutoa lugha chafu kwa wanafunzi wenzake, walimu/walezi na jamii kwa ujumla;
v. Kupigana mwanafunzi kwa mwanafunzi, kumpiga mwalimu au mtu yeyote yule;
vi. Kusuka nywele kwa mtindo usiokubalika. Wanafunzi wote wanatakiwa kuwa na nywele fupi wakati wote wawapo shuleni au kusuka kwa mtindo wa ususi uliokubalika na uongozi wa shule;
vii. Kufuga ndevu;
viii. Ulevi au unywaji wa pombe na matumizi ya dawa za kulevya;
ix. Uvutaji wa sigara;
x. Uasherati, mahusiano ya jinsi moja, kuoa au kuolewa;
xi. Kupata ujauzito au kutoa mimba;
xii. Kusababisha mimba;
xiii. Kushiriki matendo ya uhalifu, siasa na matendo yoyote yale yanayovunja sheria za nchi;
xiv. Kwenda kwenye nyumba za starehe na nyumba za kulala wageni;
xv. Kumiliki, kukutwa au kutumia simu ya mkononi katika mazingira ya shule;
xvi. Kudharau Bendera ya Taifa;
xvii. Kufanya jaribio lolote la kujiua, au kutishia kujiua kama kunywa sumu; na
xviii. Uharibifu wa mali ya umma kwa makusudi.

KARIBU SANA SHULE YA SEKONDARI NAKAGURU




Jege Lusinge Kidamila
Mkuu wa Shule

## SHULE YA SEKONDARI NAKAGURU

## FOMU YA TAARIFA BINAFSI ZA MWANAFUNZI, KUKUBALI SHERIA NA NAFASI YA SHULE ALIYOPEWA

### TAARIFA BINAFSI YA MWANAFUNZI

1. JINA LA MWANAFUNZI …………………………………………………………………
2. TAREHE YA KUZALIWA ……………………………………………………..………..
3. MAHALI ALIPOZALIWA/ MKOA/WILAYA ……………………………………………
4. MNAISHI/MNAKAA WAPI? …………………………………………………………
5. KATA/MTAA ………………………………………………………………………………..
6. URAIA MTANZANIA/SIYO MTANZANIA …………………………………………….
7. SHULE ALIKOTOKA KIDATO CHA IV ………………………………………………
8. NAMBA YA MTIHANI CSEE…………………………………………………………

### TAARIFA YA WAZAZI/ MLEZI

1. JINA LA MZAZI/MLEZI …………………………………………………………………..
2. KAZI YA MZAZI/ MLEZI …………………………………………………………………
3. ANUANI YA MZAZI/MLEZI ……………………………………………………………
4. SIMU YA MZAZI/MLEZI KAZINI ……………………… MKONONI ……………………..
   NAMBARI YA SIMU YA JIRANI YAKO NI …………………………….. KAMA HUNA
5. BARUA PEPE (E-mail) YA MZAZI/MLEZI ……………………………………………

### KUKUBALI NAFASI NA MAELEKEZO ULIYOPEWA

Mimi ……………………………………………….. kidato cha ………… mwaka……..….

Nimesoma na kuyaelewa maelekezo yote, kwa hiyo nakubali/sikubali kuipokea nafasi niliyopewa. Nathibitisha kwamba nimepokea maagizo au maelekezo bila kulazimishwa naahidi kuyazingatia.

Tarehe ………………………… saini …………………………………

### KUKUBALI SHERIA ZA SHULE MWANAFUNZI

Mimi ……………………………………………………………………………………….
nimezisoma na kuzielewa sheria za shule na ninaahidi kwamba nitazizingatia na kutii masharti, sheria za shule na maelekezo mengine nitakayopewa na mwalimu/ waalimu na viongozi wote wa shule nikizikiuka sheria hizo hatua za kindhamu zichukuliwe dhidi yangu kwa mujibu wa kanuni na taratibu na sheria zilizopo.

Tarehe ………………………………… Saini …………………………

**MZAZI/ MLEZI** (Ajaze sehemu hii)

Mimi mzazi/ mlezi wake nathibitisha kuwa mwanangu ………………………….……………. ameelewa Maagizo. Mimi mzazi/mlezi ninapenda ifahamike kuwa dini ya mwanangu ni ……………………………… na dhehebu lake ni ……………………………………………. Ninaruhusu/siruhusu mwanagu kushiriki katika makongamano au warsha za kidini nje ya shule hususani zile zinazofanyika nje ya mkoa wa Morogoro pasipo kuwa na mwalimu mlezi wa shule hii.

Ninaruhusu/siruhusu wakati wa likizo fupi atoke shuleni na kwenda kwa ……………………………………………………………………… uhusiano wake na mwanangu ni ……………………………………………………………….…………………… Namba yake ya simu ni ………………………………………………….. Aidha mimi ambaye ni mzazi/mlezi nimesoma/nimesomewa sheria na maagizo mengine ya shule yanayomhusu mwanafunzi.

Nitahakikisha namsimamia/kumgharimia kwa mahitaji yote hadi anamaliza shule

Tarehe ……………………..          Saini ………………………

# MEDICAL CERTIFICATE FORM

NAKAGURU SECONDARY SCHOOL
P. O. Box 611
IFAKARA
MOROGORO
30/04/2025

Simu: 0783 273 538
0764 232 397

To the Medical Officer,
.........................................................
..........................................................

REF: .......................................................................................................................

Please examine the above-named student as to his physical and mental fitness for being student.
Some of defect will hinder the student for Secondary Schools' Education.

1. a). Eye sight ……..……………………………………………………………………..
   b). Hearing ……..…………………………………………………………………….
   c). Limbs ………………………………………………………..…………………….
   d). Speech …………………………………………………………………………....
   e). Venereal disease …..………………………………………..…………………….
   f). Leprosy ……………………………………………………………………….….
   g). Epilepsy ……………………………………………………………...………….

2. Neurosis
……………………………………………………….……………………………………………
……………………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………

3. Other serious diseases (name them)
……………………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………

I have examined the above-named student and confirm that he is physically fit/not fit for a full time Secondary School Education.
Name..................................................................... Signature:…..............................
Date......................................
STATION...............................................................
DESINATION........................................................
N.B.

(I request this form to be returned to the school in a sealed envelope)

# NAKAGURU SECONDARY SCHOOL
# A-LEVEL BOOKS REQUIREMENT

**GEOGRAPH PAPER I**

1. Principles of Physical Geography- by F.J Monkhouse
2. A comprehensive Approach to Physical Geography for Secondary School - by D.T Msabila
3. Practical Geography for Africa by John M. Prichard
4. Land forms in Africa – An introduction to Geomorphology – by Colin Buckle 5. Africa – by J.M. Prichard
5. Practical Geography for A level – by Francis Mnyawi

**GEOGRAPH PAPER II**

1. Human and Economic Geography – by Goh cheng & Morgan
2. Advanced Level geography Course book –by Tanzania Institute of Education (TIE)
3. An Integrated Focal regional study on Human and Economic Geography Advanced level paper 2- by D.T Msabila

**PHYSICS**

1. Nelkon and Parker
2. Understanding Physics
3. Rodger Manchester
4. Calculation for A- level

**MATHEMATICS**

1. Pure mathematics Vol. 1
2. Pure mathematics Vol. 2
3. Engineering Mathematics
4. Statistics for A- level
5. Understanding Mathematics.

**CHEMISTRY**

1. Freenmentle M. Chemistry in Action. Macmillan Education Ltd. 3rd edition
2. Mzumbe Book Project: Physical Chemistry
3. Ann & Patrick- Advanced Chemistry

**BIOLOGY**

1. Taylor D., Green N & Stout G. Biological Science: 3rd edition 1 & 2
2. Robert M. B. New Biology a Functional approach 4th edition
3. Glenn and Susan. New understanding Biology 4th edition
4. S. O. Loeje – Certificate Practical Biology
5. C. Advanced Biology- Principles and Applications

Note: Knowledge is acquired through Books but Skills is Obtained by Practice. Bring with you at least two books from list above.

**NB: Kwa siku za hivi karibuni kumekuwa na utapeli (wizi kwa njia ya mitandao). Baadhi ya wazazi wamekuwa wakitumiwa ujumbe mfupi au kupigiwa simu na watu wanaojitambulisha kama walimu na kuwafahamisha kuwa mtoto wa mzazi husika ambaye ni mwanafunzi ni mgojwa na yuko mahututi hivyo mzazi atume pesa. TAFADHALI UPATAPO UJUMBE WOWOTE KUHUSU MWANAFUNZI/MTOTO WAKO USITUME CHOCHOTE, NI VEMA UKAWASILIANA NA UONGOZI WA SHULE KUPATA UKWELI WA TAARIFA HUSIKA KWA NAMBA ZIFUATAZO:**

| | |
|---|---|
| a) Mkuu wa Shule: | 0783 273 538 |
| b) Makamu Mkuu wa Shule: | 0784 169 094 |
| c) Mwandamizi Taaluma: | 0686 010 188 |
| d) Matron/Patron: | 0684 982 878 |